

# KULINDA USIKU DHIDI YA MWANGAZA

Maelekezo Matano ya Kuweka  
Mwangaza wa Nje Kiwajibifu



Illuminating  
ENGINEERING SOCIETY



## UHITAJIKE



### KUWE NA SABABU YA MAANA YA KUWEKA MWANGAZA

Kabla ya kuweka au kubadilisha taa/balbu, hakikisha kama mwangaza unahitajika. Zingatia vile mwangaza utaathiri eneo, ikiwemo wanyama mwitu na mazingira. Badala ya taa/balbu, tumia rangi za kuelekeza mwangaza, au alama zinazoangaza, kwenye ngazi na viashiria, na pia pa kutembelea.

## ULENGE



### MWANGAZA USIFIKE PASIPO HITAJIKA

Tumia vizuizi na uelekeze mwangaza ulenge pale ambapo unataka pamulikwe. Hakikisha mwangaza unaelekea chini na hautapakai ukafika pasipohitaji kuangazwa.


## UWE HAFIFU



### MWANGAZA USIWE MKALI KUZIDI INAVYOHITAJIKA

Mwangaza uwe hafifu kulingana na mahitaji. Zingatia hali ya nyuso za vitu vilivyo karibu. Hakikisha hazielekezi mwangaza mwingi angani.

## UDHIBITIWE



### MWANGAZA USIWE NYAKATI AMBAZO HAUTUMIKI

Tumia vidhibiti kama vipima-muda na vigundua-mwendo kuwashaa, kuhafifisha, na kuzima taa/balbu.

## RANGI



### EPUKA RANGI ZA MAWIMBI MAFUPI

Usiweke mwangaza wa rangi ya buluu, nili, au urujuani. Hafifisha miangaza ya rangi hizi kama ni lazima itumike.